

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



**S. L.P 1575,
Iringa.
Simu: (026) 2700157
Nukushi: (026) 2703014
Barua pepe:
rbciringa@pccb.go.tz
Mtandao : www.pccb.go.tz**

IRINGA 29 JUNI, 2020

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**TAKUKURU YAMFIKISHA MAHAKAMANI ALIYEKUWA RAIS WA
SERIKALI YA WANAFUNZI CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII
RUAHA KWA KUJIPATIA FEDHA KWA NJIA YA WIZI**

Ndugu Wanahabari,

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Iringa kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, inatarajia kumfikisha Mahakamani aliyekuwa Rais wa wanafunzi Chuo cha Maendeleo ya Jamii RUAHA (CDTI) **CHRISTOPHER MICHAEL MOLLEL** kwa makosa manne (4) yafuatayo:

- (i) Kosa la wizi wa shilingi 1,250,000/= kinyume na Kifungu cha 258(1) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 265 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 pitio la Mwaka 2002;
- (ii) Kugushi kinyume na Vifungu vya 333, 335(d) (1) na 337 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 pitio la Mwaka 2002,
- (iii) Kuwasilisha maelezo ya uongo kinyume na Kifungu cha 342 kikisomwa pamoja na Kifungu cha 337 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 pitio la Mwaka 2002 pamoja na
- (iv) Kosa la kutoa taarifa ya uongo kwa mtu aliyeajiriwa katika mamlaka ya Umma kinyume na Kifungu cha 122(a) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 pitio la Mwaka 2002.

Uchunguzi wa TAKUKURU Mkoa wa Iringa ulibaini kuwa, mnamo tarehe 25/10/2019 mtuhumiwa akiwa ndiye Rais wa Serikali ya Wanafuzi chuoni hapo alichana na kuiba hundi Namba. 000063 kutoka katika kitabu cha hundi ya **'Ruaha CDTI Students Organization'** kilichokuwa kimehifadhiwa ofisini kwa Mshauri wa Wanafunzi (Dean of Students) wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha.

- Kwamba baada ya kuiba hundi hiyo alijaza taarifa za uongo za kutakiwa kulipwa fedha kiasi cha Sh. 1,250,000/= ambapo alisaini akiwa mmoja wa watia saini katika akaunti hiyo na kughushi saini ya mtia saini (mwalimu) wa pili katika akaunti hiyo.
- Pia uchunguzi umebaini kuwa mtuhumiwa tarehe 26.10.2019 aliwasilisha hundi hiyo Namba 000063 ya akaunti **Namba 60510007147** katika Benki ya NMB Mkwawa iliyopo Iringa Mjini akiwa ameambatanisha na nakala ya kuwekea hundi ambayo ilikuwa na maelekezo ya kutoa fedha kiasi cha Sh. 1,250,000/= kutoka akaunti ya **'Ruaha CDTI Students Organization'** kwenda katika akaunti yake binafsi **Namba 6051**.

Ndugu Wanahabari,

Uchunguzi wa tuhuma hii umekamilika na TAKUKURU Mkoa wa Iringa kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka inatarajia kumfikisha mtuhumiwa Mahakamani leo Juni 29, 2020 katika Mahakama ya Wilaya ya Iringa

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa inatoa wito kwa wakazi wote wa mkoa wa Iringa kutofumbia macho wanaojihusisha na vitendo vya Rushwa na kwamba inaendelea kuwasihia kutoa taarifa sahihi kwa TAKUKURU ili hatua stahiki zichukuliwe.

Penda nchi yako, kataa rushwa.

Imetolewa na :-

Mweli Evart Kilimali,
MKUU WA TAKUKURU MKOA WA IRINGA